

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUMALIZIKA KWA MLIPUKO WA UGONJWA WA VIRUSI VYA MARBURG KATIKA WILAYA YA BIHARAMULO, MKOANI KAGERA

BIHARAMULO, 13 Machi, 2025

Ndugu Wananchi,

Tarehe 20 Januari, 2025, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitangaza uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa Virusi vya Marburg (MVD) katika Mkoa wa Kagera, ambapo wagonjwa wawili (2) walithibitika kuwa na maambukizi. Kwa masikitiko makubwa, wote wawili walipoteza maisha wakiwa kwenye matibabu. MVD ni ugonjwa hatari unaoweza kusambaa kutoka mtu mmoja hadi mwingine kupitia mgusano wa moja kwa moja na majimaji ya mwili kutoka kwa mtu aliyeambukizwa. Ikiwa hautadhibitiwa kwa wakati, unaweza kusababisha madhara makubwa ikiwa ni pamoja na vifo na athari za kijamii na kiuchumi.

Ndugu Wananchi,

Tangu kutangazwa kwa mlipuko huu, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilichukua hatua madhubuti kudhibiti na kuzuia kuenea kwa ugonjwa huu katika Halmashauri ya Biharamulo iliyoathirika. Kama ambavyo tumekuwa tukitoa taarifa za mara kwa mara kupitia vyombo vya habari na majukwaa mengine, mgonjwa wa mwisho aliyethibitika kuwa na MVD aliripotiwa tarehe 28 Januari, 2025. Kufikia tarehe 11 Machi, 2025, siku arobaini na mbili (42) zilikuwa zimepita tangu kuwepo kwa mgonjwa huyo wa mwisho. Kitaalamu na kulingana na kanuni na taratibu za Shirika la Afya Duniani WHO, tumekidhi vigezo vya kutangaza rasmi kumalizika kwa mlipuko wa MVD. Hivyo basi, leo tarehe 13 Machi, 2025, ninatangaza rasmi kumalizika kwa mlipuko wa MVD nchini.

Ndugu Wananchi,

Ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa maelekezo yake na uwezeshaji mkubwa aliofanya

ambao umepelekea kumalizika kwa ugonjwa huu. Natambua kazi kubwa iliyofanywa na jamii na wataalam walioko mstari wa mbele wakiwemo watoa huduma za afya, maafisa ustawi wa jamii, wataalamu wa lishe na wahudumu wa afya ngazi ya jamii, kwa kujitoa kwenu na utayari wenu wakati wa kukabiliana na mlipuko huu.

Ndugu Wananchi,

Vile vile, natoa shukrani zangu za dhati kwa timu ya kitaalamu inayoongozwa na Dkt. Seif Shekalaghe, Katibu Mkuu Wizara ya Afya kwa usimamizi wake mzuri hadi kufikia leo hii. Aidha, namshukuru Dkt. Grace Magembe, Mganga Mkuu wa Serikali pamoja akiwa na wajumbe kutoka Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera na Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo. Shukrani zangu za pekee pia ziende kwa wote waliohusika katika kukabiliana na mlipuko huu, wakiwemo wananchi, viongozi wa ngazi mbalimbali, watu wenye ushawishi, wadau wa maendeleo, mashirika, sekta binafsi, viongozi wa dini, waandishi wa habari, na mashirika yanayotekeleza afua za afya kwa ushirikiano na Serikali.

Ndugu Wananchi,

Nasisitiza kwa jamii yote kuendelea kuwa makini hata baada ya kutangazwa kumalizika kwa mlipuko huu, kwa kuzingatia hatua zote za kujikinga, ikiwa ni pamoja na kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono (sanitizer), kutoa taarifa kwa wakati za uvumi au tukio lolote lisilo la kawaida katika jamii kupitia namba ya dharura 199 au kituo cha afya kilicho karibu.

Aidha, tunapaswa kufahamu kuwa taifa letu bado liko kwenye hatari ya magonjwa mengine ya kuambukiza kwa kasi, ikiwa ni pamoja na Ebola ambao umeripotiwa katika nchi jirani na na Mpox unaoendelea duniani na kutangazwa kutokea nchini kwetu hivi karibuni. Hivyo basi, tunatoa wito kwa wananchi wote kuendelea kushirikiana na mamlaka za afya na kuzingatia hatua zote za kujikinga dhidi ya magonjwa hayo.

Mwisho, napenda kuwahakikishia kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kuchukua hatua stahiki kuhakikisha wananchi wake na jumuiya ya kimataifa wanabaki salama.

Imetolewa na:



Jenista J. Mhagama (MB)
WAZIRI WA AFYA